



NDUGU MSOMAJI NA MFUATILIAJI KARIBU KATIKA SEMINA ZETU ZA PEKEE
SANA ZA NENO LA MUNGU “INAWEZEKANA KUISHI MILELE”

SOMO LA KWANZA LINASEMA:

Inawezekanaje Kuishi Milele Katika Maisha ya Shida?

Fungu Kuu: “*Na uzima wa milele ndio huu wa kujue wewe, MUNGU wa pekee wa kweli, na YESU Kristo uliye mtuma*” **Yohana 17:3**

Na. Dkt. Edward Raphael Mhina

Nianze kwa kusema ya kwamba “*nampenda sana MUNGU*” kwa sababu alituumba wakamilifu sana. Ukitazama dunia jinsi alivyo iumba hakika ni ya pekee sana japo imeharibika bado lakini bado inaonekana yenye mvuto. Kwa mfano ukitazama mmea wa waridi, japo una miba mikali lakini bado limebeba ua zuri lenye harufu nzuri sana la waridi.

Napiga picha jinsi ilivyo kuwa hapo mwanzo kwa kweli najua kwa hakika ya kwamba ilikuwa nzuri na ya kupendeza sana, kwa uthibitisho huu tafakari nami kutoka katika **Mwanzo 1:31**, “*Mungu akaona KILA KITU alichokifanya, na tazama, NI CHEMA SANA. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita.*” Hakukuwa na shida zozote katika dunia wakati MUNGU mwenyezi alipoiumba na alikusudia kwamba maisha ya mwanadamu yawe ya furaha, amani na mafanikio siku zote. **Yeremia 29:1**, “*Maana nayajua MAWAZO NINAYOWAWAZIA NINYI, asema Bwana, NI MAWAZO YA AMANI WALA SI YA MABAYA...*” Hakika nakuandikia yakuwa MUNGU wetu ni MUNGU mwenye pendo kubwa sana.

Wazo kuu; sasa kwanini shida ? Shida imeingia kwa kukiuka maagizo tuliopewa na MUNGU wakati wazazi wetu wa kwanza walipokabidhiwa bustani ya Edeni. Wazazi wetu wa kwanza Adamu na Hawa walikula matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya ambalo MUNGU aliwakataza. Ukitafakari nami katika **Mwanzo 3--**inaonesha jinsi ambavyo wazazi wetu wa walishwawishiwa na shetani na kuingia katika shida(dhambi) kwa kukiuka maagizo ya Mungu. Tangu mwanzo MUNGU alikusudia binadamu wawe na akili ya ufahamu wa kutenda mema tu siku zote, lakini uchaguzi wetu umefanya tuwe katika shida hizi na matatizo tuliyo nayo kwa kuchagua kujua mema na mabaya. Ndivyo ilivyo hadi leo, kuna watu wengi sana ambao wanapitia maisha ya shida na utumwa kwa sababu wamekataa kufuata maagizo ya Mungu.

Lakini napenda kukuhabarisha ya kwamba MUNGU mwenyewe akiwa katika umbile la binadamu(*Imanueli: Imanu—Pamoja Nasi na Eli—Mungu, Tazama Mathayo 1:23*) alishuka na kufa kwa ajili ya shida hizi tulizo nazo naye aliishinda mauti ili tuwe na uzima wa milele kwa kumwamini. Ukisoma katika **Yohana 3:16** “*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na UZIMA WA MILELE.*”



Hakika kwa habari hiyo tunafanywa huru endapo tutayatoa maisha yetu na kumkabidhi YESU ili ayatawale. Leo Yesu yupo kwa ajili yako na kwa ajili yangu, maana aliyatoa maisha yake, akaacha enzi na utukufu wake mbinguni ili aje afe kwa ajili yako na kwa ajili yangu ili tuishi milele. Anasema na kusihia tena kwa upole, *“Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo(SHIDA/DHAMBI), nami nitawapumzisha.” Mathayo 11:28.* Kama leo utaisikia sauti ya Bwana itii na uungane nami kumfuata, wala usiufanye moyo wako kuwa mgumu. Kumbuka kupitia kujitoa maisha yetu kwake, anatufanya viumbe vipya, hutuondolea shida zitusumbuazo na kufanya iwezekane kuishi milele maisha ya furaha, amani na mafanikio.

Kama umebarikiwa sali nami sala hii.....:

“Nimejua ya kwamba shida zote zinazo nipata ni sababu sijayatoa maisha yangu kwako, rafiki yangu mpendwa na BABA yangu MTAKATIFU MUNGU uishie milele zote, ninakubali nimekutenda dhambi, nisamehe dhambi zangu, nipe moyo wa kujifunza zaidi Neno lako, kwa jina la YESU KRISTO AMEN.”

KARIBU TENA KATIKA SOMO LIJALO LINALO SEMA:

“Inawezekanaje Kuishi Milele Wakati Kuna Kifo? Je, Wafu Wapo Wapi?”

Maswali, Maoni au Ushauri wasiliana nami: +255652648737 au +255768678122